Huzuni ya Dunia Na Huzuni ya Mungu
(Worldly Sorrow And Godly Sorrow)

Na

Ellis P. Forsman

Huzuni ya Dunia Na Huzuni ya Mungu
(Worldly Sorrow And Godly Sorrow)

Na

Ellis P. Forsman

Agosti 11, 2018

Huzuni ya Dunia Na Huzuni ya Mungu

2 Kor. 7:10

2 Kor. 7:10, "*Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Munguhufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti.*"

Kifungu hiki kinatuonyesha toba ya kweli. Inaonekana kwamba mwanadamu amekuwa na wakati mgumu na toba. Anataka wokovu, anazitubia baadhi ya dhambi, na kuacha zingine.

Ni mhimu kwetu kujua toba ya kweli ni nini na kuifanya tunapotenda dhambi.

Sasa tuangalie huzuni ya dunia na huzuni ya Mungu:

Huzuni ya dunia

Wapo wengi wanao lia kwa sababu ya hali zao, siyo kwa sababu ya kumpenda Mungu. Ikiwa vitu katika dunia vimebadilika wasingekuwa wanalia hata kidogo. Wanajihurumia wenyewe badala ya kusumbuka kuhusu heshima na ukuu wa Mungu ambaye walimchoma zamani. Wanapenda waondolewe katika mkwamo wao, lakini si katika njia inayoleta utukufu kwa Mungu.

Kuna mifano mingi ya aina hii ya huzuni. (machozi ya Esau, toba ya Farao, huzuni ya kijana tajiri).

Nabii Yoeli alisema haya kwa watu waliotaka kutubu.

Yoeli 2:13, "*Rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu, makamrudie BWANA Mungu wenu kwa maana yeye ndiye mwenye neema, amejaa huruma si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa huruma, naye hughairi mabaya.*"

Ni alama gani ambazo ni za huzuni ya dunia?

Huzuni ya dunia huja kwa uelewa wa mwanadamu kwa uvunjifu wa sheria. (Kupatwa ukiwa kasi). Kadiri muda unavyokwenda, anaweza kutaka kununu kifaa ambacho kitamuonya wakati kifaa cha polisi kikiwa kimewashwa, hivyo anaweza kuendeleza mwendo kasi.

Huzuni ya dunia hukaa katika mipango ambayo mwanadamu anapanga. Mwanadamu anataka kuishi kidunia na maisha ya dhambi, lakini afadhali ifanyie kazi kama kwenda mbinguni ndio mwisho.

Wengine wanahuzunika kwa dhambi zao na wengine kwa wakati huo hutubu, lakini sio kwa muda mrefu.

Huzuni ya dunia hutokana na wanadamu kuacha njia nyingi za dhambi, lakini sio kuchukizwa na kugeuza migongo yao kwa dhambi yenyewe. Wengine hubadili kilevi moja baada ya nyingine. Mtu anaweza kuchukia kuapa, lakini akadanganya katika ushuru wa kipato chake.

Huzuni ya dunia umuacha mwanadamu bila uwezo wa kushinda majaribu. Huzuni ya dunia ni kugeuka kutoka katika dhambi zako; husimama kifupi katika kugeuka kiimani kwa Kristo.

Huzuni ya dunia humsababisha mtu atafute msaada kwa watu wengine. Ameshindwa na maisha na anamtafta daktari, daaktari wa akili, mshauri, au yeyote atakayekuwa mbadala wa Kristo.

Huzuni ya dunia humpeleka mtu katika mauti (upotevu wa nafsi).

Huzuni ya Mungu huongoza katika wokovu

2 Kor. 7:10, "*Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Munguhufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti.*"

Huzuni ya Mungu huleta ufahamu wa toba, sio tu kugeuka kutoka katika dhambi zetu, lakini kutoka katika dhambi zetu, kutubu kweli.

Lazima tufike katika mizizi ya dhambi. Toba ya kweli huanzia na kuwa na huzuni kwamba umemuudhi Mungu. (Isipokuwa, hiyo ni, hakuna toba ya kweli itakayokuja.)

Zingatia maelezo haya ya toba ya kweli:

Mfalme Daudi. Zaburi 51:1-19, "*Ee Mungu, unirehemu, sawasawa na fadhili zako. Kiasi cha wingi wa rehema zako, uyafute makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, unitakase dhambi zangu. Maana nimejua mimi makosa yangu na dhambi yangu I mbele yangu daima. Nimekutenda dhambi wewe peke yako, na kufanya maovu mbele za macho yako. Wewe ujulikane kuwa unahaki unenapo, na kuwa safi utoapo hukumu. Tazama mimi naliumbwa katika hali ya uovu; mama yangu alinichukua mimba hatiani. Tazama, wapendezwa na kweli iliyo moyoni; nawe utanijulisha hekima kwa siri, unisafishe kwa hisopo nami nitakuwa safi, unioshe nami nitakuwa mweupe kuliko theluji unifanye kusikia furaha na shangwe, mifupa uliyoiponda ifurahi. Usitiri uso wako usitazame dhambi zangu; uzifute hatia zangu zote. Ee Mungu, uniumbie moyo safiuifanye upya roho iliyotulia ndani yangu usinitenge na uso wako, wala roho wako mtakatifu usiniondolee. Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya wepesi. Nitawafundisha wakosaji njia zako, na wenye dhambi watarejea kwako. Ee MUNGU, Mungu wa wokovu wangu, uniponye na damu za watu, na ulimi wangu utaiimba haki yako. Ee Bwana uifumbue*

midomo yangu, na kinywa change kitazinena sifa zako. Maana hupendezwi na dhabihu, au ningeitoa, wewe huridhii sadaka ya kuteketezwa. Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau. Uitendee mema Sayuni kwa radhi yako, uzijenge kuta za Yerusalemu. Ndipo utakapopendezwa na dhabihu za haki, na sadaka za kuteketezwa, na kafara. Ndipo watakapotoa ng'ombe juu ya madhabahu yako."

Mwana mpotevu. Luka 15:18, "*Nitaondoka nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako.*"

Huzuni ya Mungu huleta badiliko – kutoka dhambini hadi katika maisha ya haki.

Toba iliyoletwa na huzuni ya kiungu hutazamwa katika dhambi zetu, na pia kwa Mwokozi, Yesu Kristo. (Kutaka kumpendeza). Huzuni ya Mungu huleta toba inayomuongoza mtu kuamini katika Mwokozi. (Kuacha). Mtu hugeuza maisha yake juu ya Kristo, kwa mwongozo wake (awe mtakatifu au mwenye dhambi).

Toba kama hiyo huongoza kuiweka dhambi katika mauti.

Kol. 3:1-8, "*Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu. Basi vivisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu; kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu. Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani, mlipoishi katika hayo. Lakini sasa yawekeni mbaya haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu.*"

Hitimisho

Kuzitubia baadhi ya dhambi na kuacha zingine siyo toba ya Mungu.

Kuwa na huzuni kwamba dhambi zetu zimefunuliwa ni huzuni ya dunia.

Toba ya kweli hujumuisha kuingia katika mzizi wa dhambi, kwa kuhuzunika kwamba umemuumiza Mungu, na kumuachia Mungu maisha yako mara tena.

Je unahitaji kutubu?